

Kufungamana kwa Vitendawili vya Wanyakyusa na Matukio ya Kijamii

Gerephace Mwangosi

Idara ya Lugha, Chuo Kikuu cha Kikatoliki Ruaha

Email: mwangosigerephace@yahoo.com

Ikisiri

Makala haya yanahusu jinsi vitendawili vya Wanyakyusa vinavyosawiri na kufungamana na mabadiliko yanayotokea katika muktadha halisi wa jamii hiyo. Data ya makala haya ilikusanywa makaazini kwa mbinu ya mahojiano na hojaji ambapo utafiti ulifanyika katika wilaya ya Rungwe. Nadharia iliyotumika ni ile ya Uhistoria Mpya. Kanuni ya msingi katika nadharia hii ni kuitalii fasihi, na kuikita katika muktadha wa kihistoria na kuuelewa utamaduni na historia yake kupitia kazi za kifasihi. Historia ya jamii ni zao la utamaduni mahususi kwa kuyachukua matukio ya kihistoria na kuyafanya sehemu ya kazi ya fasihi (Abrams, 1999; Wamitila, 2002; Selden na wenzake, 2005). Kwa jumla makala haya, yanalenga kuchambua vitendawili vya Wanyakyusa vinavyofungamana na matukio ya kijamii.

Utangulizi

Lugha ya Kinyakyusa ni miongoni mwa lugha zinazozungumzwa nchini Tanzania, hasa eneo la Nyanda za Juu Kusini, mkoani Mbeya. Kinyakyusa, kwa mujibu wa Bleek (1862) na Guthrie (1948), ni lugha ya Kibantu. Pia, wanaeleza kuwa lugha ya Kinyakyusa ina lahaja mbili ambazo ni Kingonde inayozungumzwa na wakazi wa tambarare za ziwa Nyasa (wilaya ya Kyela), na lahaja ya pili ni Kimwamba inayozungumzwa na wakazi wa milimani (wilaya za Rungwe). Lahaja ya Kimwamba ndiyo ambayo tumeifanyia utafiti katika makala haya.

Meyer (1993) anaeleza kuwa, Wanyakyusa wanakisiwa kuwa walianza kuingia Unyakyusa ya leo mwaka 1600 BK wakitokea Mahenge, Morogoro. Katika Mradi wa Lugha Tanzania (2009) imeelezwa kuwa jumla ya Wanyakyusa ni 682,539.

Hawa wanaishi mkoani Mbeya katika wilaya ya Rungwe. Kama ilivyo kwa jamii nyinginezo barani Afrika, jamii ya Wanyakyusa ina utamaduni wake ambao umejikita zaidi katika fasihi simulizi tangu zama za maisha ya mwanadamu (Meyer, 1993).

Kwa mujibu wa Nkwera (2002) vitendawili ni kipera kimojawapo cha fasihi simulizi. Vitendawili vya jamii ya Wanyakyusa hujulikana kama *Ubupingamu* kwa maana ya kitu, jambo au suala ambalo linaelezwa kwa namna isiyo wazi. Maana hii haina tofauti na zile zinazoelezwa na wataalamu wengine kama vile; Wamitila (2002), Nkwera (2002), Mulokozi (1996) na Senkoro (1985) ambao wanaeleza kuwa, vitendawili ni maneno yanayoficha maana ya kitu kisijulikane kwa urahisi. Kwa jumla, utegaji na uteguaji wake unategemea sana ubunifu, na muktadha unaozingatia mabadiliko ya jamii na wakati. Kwa kuwa jamii ya Wanyakyusa inakua, inabadilika na hata kuingiza fikra mpya, hapana shaka kuwa maudhui ya vitendawili yanabadilika kulingana na ujuzi wa fikra, mwamko na changamoto za jamii hiyo.

Mwansoko (1988) na Khatibu (1990) wanaeleza kuwa, vitendawili sio kitu kilichosimama tu bila kuathiriwa na mabadiliko ya kijamii kwa kuzingatia wakati, historia, jiografia, utamaduni, siasa na uchumi. Kwa maoni yetu, siyo rahisi kwa jamii ya Wanyakyusa kuukwepa mkondo wa mabadiliko yatokeayo ndani na nje ya nchi. Aidha, hapana shaka kuwa, mabadiliko yanayotokea katika jamii yanaweza kuleta changamoto mbalimbali katika utanzu wa vitendawili kwa kuwa ni zao la jamii (Kirumbi, 1977).

Kwa jumla, maelezo yaliyotolewa na Kirumbi, Mwansoko na Khatibu hapo juu, ndiyo yanayojenga msingi wa lengo la makala haya yanayochunguza uhusiano kati ya vitendawili na mabadiliko yanayotokea katika jamii ambayo yanachangia kuibua vitendawili vinavyosadifu muktadha wa jamii ya Wanyakyusa.

Vitendawili na Maudhui Yake

Senkoro (1982) anaeleza kuwa, maudhui ya kazi za fasihi hujumuisha mawazo, pamoja na mafunzo ambayo

yamemsukuma mtunzi au msanii hadi akatunga, na kusana kazi ya sanaa. Ndani ya maudhui kuna vipengele kama vile; migogoro, ujumbe, falsafa na mtazamo. Katika makala haya, tumechambua namna dhamira za vitendawili vya jamii ya Wanyakyusa vinavyofungamana na matukio ya kijamii inayohusika. Sehemu ifuatayo inahusu uchambuzi wa dhamira za vitendawili vya Wanyakyusa vitokanavyo na matukio ya kijamii.

Uchambuzi wa Dhamira za Vitendawili vya Wanyakyusa

Tanzania imekumbwa na mabadiliko makubwa ya kiuchumi, kisiasa na kiutamaduni tangu miaka ya 1980. Mabadiliko hayo yametokana na msukumo unaotokea katika mataifa mengine (Taasisi ya Elimu, 2004). Utandawazi ni moja kati ya mambo yanayochangia mabadiliko hayo, hasa katika nchi za ulimwengu wa tatu, ikiwemo Tanzania. Kwa kuwa utandawazi hauna mipaka, ni dhahiri kwamba, hata dhamira za vitendawili zinahusiano mkubwa na mabadiliko yanayojitokeza katika jamii kama ilivyo katika nyanja nyingine. Kwa hiyo, katika sehemu inayofuata, tumeeleza baadhi ya dhamira zinazojitokeza katika vitendawili vya Wanyakyusa vitokanavyo na matukio ya kijamii.

Vitendawili Vinavyosawiri Mauaji ya Albino

Kwa mujibu wa maelezo ya watafitiwa, kabla ya miaka ya 1980 wakazi wa Rungwe walikumbwa na tatizo la kuvamiwa na wanyama wakali, hususani chui kutokana na eneo hilo kuzungukwa na vichaka na misitu iliyoko katika safu za milima Rungwe, Uporato, Kyejo na Ukinga (Livingstone). Mara kwa mara mifugo, na watu walivamiwa na hata kuuawa. Jamii iliishi kwa wasiwasi kwa kuwa uvamizi ulikuwa hautabiriki. Tatizo hili linalinganishwa na hali ya mauaji ya Albino, uchunaji wa ngozi za binadamu, hasa watoto ulioshamiri sehemu mbalimbali za nchi, likiwemo eneo la Wanyakyusa. Wauaji wa watoto na Albino wanalinganishwa na harakati za chui waliowasakama mara kwa mara katika kaya zao, na hata wakiwa katika shughuli zao za uzalishaji mali.

Makala haya yalibaini vitendawili vinavyosawiri na kuonesha hatua mbaya aliyofikia binadamu kwa kumuua binadamu

[Ruaha Journal of Arts and Social Sciences Vol 2, 2016](#)

mwenzake hasa ukizingatia mauaji ya watoto na Albino katika jamii ya Wanyakyusa. Baadhi ya vitendawili hivyo ni kama hivi vifuatavyo: “*Imibhole ghikhelilwe mumbingilo*” (*Abhabwuta abhasakalijha na abhanini*). [Chui wametapakaa katika jamii - Wauaji wa Albino na watoto]. “*Kyajepo gwaghanile nikinyamana*” pamoja “*Iminyamana gikhuponjolana*” (*Abhabhuti*). [Afadhali ukutane na chui - Wauaji wa watu]. Sababu kubwa ya mauaji hayo, kwa mujibu wa watafitiwa ni kuwepo kwa imani za kishirikina zinazohusiana na masuala ya kibiashara. Vitendawili hivi vinaitikia harakati za taifa za kukomesha mauaji ya wazee, watoto na Albino, kutokana na kushamiri imani potofu katika kipindi hiki cha utandawazi katika jamii.

Pia, makala haya yalibaini namna suala la kuuawa kwa Albino lilivyofumbiwa macho kabla ya miaka ya 1980, kwani watoto hasa vijana, walijengewa imani na dhana ambayo kimsingi ilipotosha ukweli kuwa Albino hawafi ila wanapotea, na kwamba wanakwenda kuishi mahali pengine pasipojulikana, kama kitendawili hiki kisemacho; “*Ijholo bhatighi bhatikufwa loli bhikhujhonge nkambofi*” (*Abhasakhalijha*). [Zamani tuliambiwa hawafi ila wanapotea na kwenda kuishi mahali pasipojulikana – Albino]. Hali hii ililenga kuficha aibu ya unyama huu ili usijulikane kwa jamii, jamii za mataifa mengineyo duniani. Kwa namna nyingine, hali hii ilikuwa inahalalisha mauaji ya Albino kuwa endelevu, pamoja na kukosekana kwa hatua madhubuti za kukomesha mauaji hayo.

Vitendawili Vinavyosawiri Maradhi Katika Jamii

UKIMWI kwa sasa ni janga la taifa, kama Pastore (1993) anavyoeleza kuwa, UKIMWI unaiangamiza Jamii, kwani hauchagui mkubwa wala mdogo. UKIMWI ni miongoni mwa masuala yaliyoitikisa jamii ya Wanyakyusa kutoka na maafa yanayotokana na tatizo hilo. Baadhi ya vitendawili vinavyosawiri hali hii, ni hiki kisemacho; “*Ukulya amasisa*” (*Unkota ugwakongelapoubhumi*). [Anakula mashudu - Dawa za kupunguza makali ya ugonjwa wa UKIMWI]. Mashudu ni machicha yanayopatikana baada ya kukamua mafuta ya alizeti na pamba. Mashudu yanatumika kulishia wanyama na kuwafanya wanenepe sana. Mashudu yanalinganishwa na

[Ruaha Journal of Arts and Social Sciences Vol 2, 2016](#)

dawa anazopata muathirika wa UKIMWI ili kupunguza makali ya UKIMWI, pamoja na magonjwa nyemelezi. Baadhi ya watafitiwa walieleza kwamba, hali ya kuendelea kutumia dawa za kupunguza makali ya UKIMWI kumechangia maambukizi kuwa endelevu zaidi. Kitendawili hiki kinaonesha matumaini kwa mtu aliyeathirika kwa UKIMWI

Baadhi ya vitendawili vinavyosawiri suala la mapambano dhidi ya UKIMWI, na kuonesha jinsi maambukizi yalivyoshika kasi kutokana na kukosekana kwa elimu mahususi inaeleza, na kufafanua kwa kina chanzo, kuenea na athari zake hapa nchini. Kwa mfano: “*Unkota gwa lughano gwutwabwile*” (*Inyambi*). [Dawa ya penzi imetunusuru – Kondomu] na “*Ingwegho jibhateghelile abhatubwa*” (*Ubhuhesya*). [Mkuki unawanyemelea vijana – UKIMWI]. Kondomu inatumika kama kinga dhidi ya maambukizi ya UKIMWI. Mkuki unalinganishwa na nguvu za urijali. Nguvu hizo ndizo zinawatumbukiza vijana walio wengi katika maambukizi kutokana ngono zembe au kufanya mapenzi bila kinga, ama tahadhari. Mkuki ni miongoni mwa silaha za jadi zilizotegemewa katika harakati za kupambana na maadui. Silaha hii inalinganishwa na namna UKIMWI unavyoangamiza jamii hasa vijana. UKIMWI kwa sasa ni hatari kwa ustawi wa maisha ya watu, taifa na maendeleo yake .

Mutembei (2005 na 2009) anasawiri hali ya maafa kama anavyoeleza kuwa, janga la UKIMWI limeleta changamoto mbalimbali duniani kote, na jinsi watu wanavyohusisha UKIMWI na imani za kishirikina na ushetani. Kwa mfano: “*Ubhubhine ubhu bhatwele abhalosi abhakhunguluka*” (*Ubhuhesya*). [Ugonjwa ulioletwa na wachawi – UKIMWI]. Mpaka sasa katika miaka hii ya 2000, wapo wanaoamini kuwa UKIMWI ni ugonjwa unaoletwa na wachawi ili kuwaangamiza vijana waliokuwa wanaishi mjini. Kushamiri kwa imani za kishirikana kumechangia jamii kupuuza harakati za kupambana na UKIMWI kikamilifu, mathalini, kutumia kondomu.

Tehenan (2003) anaeleza kuwa Shirika la Afya la Dunia linaeleza kwamba, kuchanganyikiwa ni tatizo linaloshika nafasi ya pili kusababisha vifo, na kuathiri uwezo wa watu kuwajibika katika nchi zinazoendelea kufikia mwaka 2020.

Baadhi ya vitendawili vyenye kusawiri hali hii ni: “*Abhalosi bheghile amahala ghosa*” (*Ukusobha amahala*). [Wachawi wamechukua akili zote–Kuchanganyikiwa]“*Ulupapike lujhughanike*”(*Ukhusobha amahala*). [Ungo umetikisika – kuchanganyikiwa]. Ungo au dishi ni dhana inayolinganishwa na chombo kinachodhibiti mfumo wa mawasiliano katika televisheni. Hali inasababishwa na vijana kupenda kutumia madawa ya kulevya yaliyo katika mfumo wa unga, vidonge na kuchoma sindano. Aidha, inatokana na kufiwa, kupoteza kazi, kufilisika na ulevi wa kupindukia wa matumizi ya pombe za kisasa, na kijadi. Haya ni baadhi ya mambo yanayosababisha kuchanganyikiwa. Baadhi ya watafitiwa walitoa maoni yao kuwa katika karne hii ya 21, haipendezi kuamini kwamba, nguvu yoyote tusiojua ina maana ya uchawi.

Vitendawili Vinavyosawiri Uwekezaji wa Kigeni hapa Nchini

Makala haya yanaonesha baadhi ya vitendawili vya Kinyakyusa vinavyohusiana na masuala ya uwekezaji hapa nchini. Kwa mfano: “*Abhakangali bikhunuelaiwefwe ubwalwa nkapuulwe*” (*Abhakilusi abhajanga*). [Wazee wanakunywa pombe kwenye kibuyu kwa kutumia mirija - Wawekezaji wa kigeni], “*Bhikhututula kuno bhikhutonga ilopa*” (*Abhakilusi abhahesya*). [Wanatusaidia huku wanatunyonya damu - Wawekezaji wa kigeni]. Mirija inamaanisha mianya inayotumiwa na wawekezaji wa kigeni kunyonya na kupora rasilimali za umma hapa nchini. Madhara ya uwekezaji hasa kwa jamii ya Wanyakyusa yamejidhirisha katika ubinafsishaji wa mashamba ya chai na viwanda vya chai vya Mwakaleli, Chivanje na Katumba; na kiwanda cha gesi cha Kyejo Mwakaleli, vyote vipo wilayani Rungwe. Uwekezaji katika maeneo hayo, kwa mujibu wa watatiwa, hauna tija kwa wazawa. Aidha, ubinafsishaji umeonesha nguvu ya kuwateka viongozi wa nchi hii, na kuwafanya wakose kauli ya kukemea ama kukabiliana na harakati hasi za wawekezaji wa kigeni, mathalani, kupora rasilimali za umma na kupitia miradi isiyo na tija kwa wazawa.

Vitendawili Vinavyosawiri Suala la Siasa Hapa Nchini

Kwa mujibu wa Taasisi ya Elimu (2004), harakati za mageuzi ya mfumo wa siasa kutoka chama kimoja hadi vyama vingi vya siasa hapa nchini, zilifuata katiba ambapo Chama Cha Mapinduzi (CCM) kupitia vikao vyake, kilipitisha sera ya mageuzi mwaka 1990 ya kuanzisha mfumo wa vyama vingi vya siasa hapa nchini. Katika makala haya, vipo vitendawili vinavyosawiri hali ya mfumo wa mageuzi ya kisiasa yaliyotokana na hali ya mabadiliko duniani. Kwa mfano: *“Imipiki gyangughilinyani limolimo, palema ghamo ghalinipendi sikindile jimo” (Ibhendela)*. [Miti yangu ina jani moja moja, baadhi ya majani yana rangi zaidi ya moja – Bendera] na *“Alijekhile, lino potukhete amatingo ghake linga ghikhuntula” (Ikyibhughutula ikyalusyetulo)*. [Alizoea, sasa tuone kama kiburi kitamsaidia - Chama Cha Mapinduzi]. Majani yametumika kisanaa kumaanisha bendera za vyama vya kisiasa vilivyoshamiri hapa nchini, kama vile; CHADEMA, CCM, TADEA, NCCR-MAGEUZI na CUF. Kuwepo kwa mfumo wa vyama vingi vya kisiasa hapa nchini, kumesaidia kukua kwa demokrasia ndani ya vyama vinavyohusika, pamoja na uwajibikaji ndani ya serikali. Wananchi wanapata fursa ya uhuru wa kutoa maoni, na kuhoji masuala ya msingi yahasuyo taifa lao kupitia uwakilishi, ingawa zipo changamoto kadha wa kadha zinazotokana na kuwepo kwa mfumo wa vyama vingi vya kisiasa.

Aidha, vipo vitendawili vinavyorejea uchaguzi mkuu wa taifa uliofanyika mwaka 1985 hapa nchini, chini ya chama kimoja (CCM) kuwa ulionesha udhaifu wa kukosekana kwa demokrasia, ambapo nafasi ya kiti cha Rais wa Jamhuri ya Muungano aligombea mtu mmoja dhidi ya kivuli, upande wa pili. Kwa mfano: *“Imomma lilwilile ikhikota ningita” (Umundu ukhulwila ubhulongosi nunsyunguli)*. [Jiwe limepambana na ng’ombe dume - Mtu kugombea nafasi ya uongozi na kivuli]. Jiwe limepewa nafasi ya kupambana na dume (mtu) ili kukejeli utaratibu wa kuwa na mgombea pekee, ambao unawanyima demokrasia ya kumpata kiongozi wa nchi kwa njia sahihi na wazi. Kitendawili hiki kinasisitiza kuwepo kwa fursa sawa katika kuwania nafasi

[Ruaha Journal of Arts and Social Sciences Vol 2, 2016](#)

mbalimbali za vyama, na serikali kwa kuzingatia katiba na sheria zilizopo, haki na demokrasia.

Vitendawili Vinavyosawiri Hali ya Umaskini katika Jamii

TUKI (2004) wanaeleza kwamba, umaskini ni hali ya kukosa mali, ufukara na ukata. Umaskini ni majowapo ya matatizo yanaozikabili jamii mbalimbali hapa nchini. Katika jamii ya Wanyakyusa, vipo vitendawili vinavyohakiki tatizo hili. Kwa mfano: *“Bhutolwe bwa bhakangali kangi khaliti khasumo khabhenekhisu ukhufumalijolo”* (Ubhulondo). [Janga la wazee tangu kale - Ufukara] *“Kighune kya Kyala”* (Ubhufweje). [Laana ya Mungu – Ufukara] na *“Imbembe jangu jiswile imbondanya”* (Ubwalwa mumbembe). [Chupa yangu imejaa sumu - Chupa yenye pombe]. Ufukara ni miongoni mwa matatizo ambayo ni endelevu katika jamii tangu kale, na unatazamwa kama laana kutoka kwa Mungu, hasa kwa familia maskini. Ulevi katika jamii ya Wanyakyusa unaangaliwa kama mojawapo ya vyanzo vya umaskini kwa kuwa unapewa kipaumbele kuliko shughuli za uzalishaji mali.

Kilimo ni miongoni mwa mambo yaliyopewa kipaumbele katika serikali ya awamu ya nne ya serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ili kupambana na umaskini hapa nchini. Katika jamii ya Wanyakyusa vipo vitendawili vinavyosawiri hali hii, kwa mfano: *“Umundu ikhukhuta kukyalo”* (Ikipapatila). [Mtu analia shambani – Pawatila]. Pawatila ni trekta dogo litumikalo kulimia ambalo linalinganishwa na harakati za mkulima akiwa katika mbalimbali za kilimo. . Matumizi ya zana za kisasa kama matrekta (*power tiller*) ni jitihada mojawapo ya kuondokana na jembe la mkono ili kupambana na umaskini hapa nchini. Suala la umoja na ushirikiano katika jamii ya Wanyakyusa linatazamwa kama nyenzo ya msingi katika kupambana na umaskini. Jambo hili linajidhihirisha katika kitendawili kisemacho: *“Ndinabhanangu bhatatu linga asokhilepo jumo bhosyonangike syosa”* (Amagurutumu agha kitukutu). [Nina wanangu watatu akiondoka mmoja mambo yameharibika - Magurudumu ya Bajaji]. Kukosekana kwa gurudumu moja katikapikipiki aina ya bajaji, haiwezi kufanya kazi. Matumizi ya bajaji kama chombo cha kusafiria ni ya hivi

[Ruaha Journal of Arts and Social Sciences Vol 2, 2016](#)

karibuni katika maendeleo ya Wanyakyusa, na kujitokeza kwake katika vitendawili, kunasisitiza umuhimu wa ushirikiano hasa katika shughuli za uzalishaji mali na uchumi, pamoja na mambo mengineyo ya kijamii.

Vitendawili Vinavyosawiri Utamaduni na Changamoto za Kigeni

Utamaduni ni mila, asili, jadi na desturi za kundi la jamii fulani (TUKI, 2004). Utamaduni ni jumla ya mambo yote yanayobuniwa na jamii ili kukidhi utashi na maendeleo yake, pamoja na mwenendo wa maisha ya jamii, mtazamo wao wa mambo, na taratibu zao za kuendesha maisha zinazowatofautisha wao na jamii nyingine.

Taasisi ya Elimu (1977) wanasisitiza kuwa, taifa lenye uwezo wa kulinda utamaduni wake ni taifa kamili. Jamii ya Wanyakyusa inavyo vitendawili ambavyo vinabainisha madhara ya matumizi makubwa ya vitu vya kigeni kuliko vya ndani, kama vile; kujichubua kwa kutumia mafuta makali, yakiwemo madawa ya kuongeza ukubwa wa matiti, na makalio. Hali hii inaonesha uwezo wa taifa wa kulinda utamaduni wake wa asili, kuwa umeanza kupotea. Kwa mfano; *“Alile ikhisyesye ikhikhifumile khunja / mbhulajha”* (*Imikhota igyakhongela amabhele ne fyima*). [Ameshiba mikate ya Ulaya - Madawa ya kunenepesha matiti na makalio]. Mikate imetumika kisanaa kuonesha baadhi ya madawa yanayotoka katika nchi za kigeni hasa Ulaya na Asia (nchini China) ambayo yanatumika kuongeza ukubwa wa viungo vya mwili wa binadamu, kama matiti na makalio. Wanawake katika jamii ya Wanyakyusa, ndio watumiaji wakubwa, kwa kuwa wanaamini kuwa ni sehemu ya urembo.

Ngoma za jadi ni miongoni mwa utamaduni unaokabaliwa na changamoto mbalimbali kutokana na kushamiri kwa tamaduni za kigeni, ambazo zinaonekana kuwa na nguvu katika matumizi ya magitaa, televisheni, redio, pamoja na dini ya Kikristo inayohusisha ngoma na dhambi. Mabadiliko na changamoto zinajitokeza katika jamii zinasawiriwa katika vitendawili. Kwa mfano: *“Atutwele nakhuno tukhamanyako”* (*Ighalasi lyabhasungu*). [Ametufikisha hata ambako hatukukujua - Televisheni]. Matumizi ya televisheni ni ya hivi karibuni katika jamii ya Wanyakyusa kuanzia miaka ya 2000

hasa baada ya kupata nishati ya umeme. Licha ya hatua hii kuwa ya kimaendeleo, imechangia kufifiza utamaduni wa jadi, kama vile; ngoma, vitendawili na nyimbo,. Kitendawili hiki kinaonesha changamoto za utamaduni wa kigeni unavyoitikiwa kwa nguvu, na kuonekana wenye tija kuliko utamaduni wa jadi.

Vitendawili Vinavyosawiri Suala la Elimu Hapa Nchini

Elimu ni taaluma pekee katika jamii inayogusa nyanja zote za maisha ya binadamu. Elimu ni msingi wa maendeleo ya jamii. Hili limesisitizwa hata katika Ahadi ya Sita ya TANU ya mwaka 1962: “Nitajielimisha kwa kadri ya uwezo wangu, na kutumia elimu yangu kwa faida ya wote.” Kwa mfano: “*Abhopile indungwa*”. (*Umundu ujhualekhile, khangi akhanile ukhumanyila isukhulu*), na “*Kholelela ubhutwa bwabhasungu*” (*Imanyisyo*) [Shikilia ufalme wa Wazungu – Elimu] na “*Ungete ngubhule*” (*Ikhalata*). [Niambie nikuambie - Gazeti / Kitabu]. Lema na wenzake (2004) wanaeleza kuwa, elimu haina budi kuwaongezea watu uhuru wao wa kimwili na kifikra, na kuweza kujiongoza wenyewe katika maisha, na mazingira wanamoishi. Maendeleo ya sayansi na teknolojia katika nchi za viwanda, kama vile; Ulaya na Marekani, yametokana na elimu kupewa kipaumbele. Elimu ndicho kiini pekee cha kukabiliana na mageuzi makubwa ya siasa na uchumi wa nchi.

Hitimisho

Makala haya, yamedhihirisha na kuonesha uhusiano mkubwa kati ya vitendawili na matukio yatokeayo katika jamii ya Wanyakyusa. Kwa jumla, vitendawili vinasawiri mabadiliko yatokeayo, na kufungamana na muktadha halisi wa jamii inayohusika. Usawiri huu, hukifanya kipera cha kitendawili kukidhi na kuonesha uhai wa kumudu changamoto za kijamii kwa kadri jamii inavyokua na kubadilika, kutokana na mifumo halisi ya muktadha wa jamii iliyochunguzwa.

Kwa jumla, fasihi simulizi, na kwa hapa vitendawili, vimetupatia picha kuwa, dhamira zake, zinakidhi matakwa ya jamii, na kuwa ni kiungo muhimu katika kujenga misingi ya kuelimisha na kuburudisha, kuifahamu jamii fulani, kujua historia ya jamii, na mabadiliko yaliyojitokeza katika mikondo ya uchumi na siasa na kiutamaduni. Pia, makala haya yameonesha kuwa mabadiliko ya kisiasa na kiuchumi, mwingiliano wa jamii na maendeleo ya sayansi

[Ruaha Journal of Arts and Social Sciences Vol 2, 2016](#)

na teknolojia ni nyenzo muhimu katika kusanifu dhamira za vitendawili vinavyohakiki matukio ya kijamii.

Marejeleo

Abrams, M. H. (1999). *A Glossary of Literary Terms*. Seventh Edition. Harcourt & Brace, New York.

Bleek, W. H. I. (1962). *A Comparative Grammar of South African Languages*. Trubener & Co, London.

Guthrie, M. (1948). *Classification of Bantu Languages*. New Work Publishers for the International African Institute of O. U. P, London.

Khatibu, M. S. (1990). Vitendawili, Fani ya Fasihi Simulizi. Mulika Na. 13: Chuo, TUKI, Kikuu cha Dar es Salaam.

Kirumbi, P. S. (1977). *Misingi ya Fasihi Simulizi*. Shungwa Publishers, Nairobi.

Lema, E. na wenzake (2004). *Nyerere Kuhusu Elimu, Selected Essays and Speeches 1954 1992*. E &D Limited, Dar es Salaam.

Meyer, T. (1993). *Wakonde*. Peramiho Printing Press, Songea

Mutembei, A. K. (2005). *Kisiki Kikavu*. E&D Limited, Dar Es Salaam.

Mutembei, A. K. (2009) .*UKIMWI katika Fasihi ya Kiswahili 1982-2006*. TATAKI, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Mwansoko, H. J. M. (1988). Mbinu za Uchambuzi wa Vitendawili. Mulika Na.20, TUKI, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

- Pastore, L. J. (1993). *Comforting Aids Through Literature*. University of Illinois America.
- Senkoro, F. E. M. K. (1985). Vitendawili Katika Jamii, Maana, Maudhui naMatumizi Yake. *Mulika* na. 17; TUKI, Dar es Salaam.
- Taasisi ya Elimu, (1977). *Historia ya Tanzania Kabla ya Mwaka 1880*. Print Pak/ Mtuu, Dar es Salaam.
- Taasisi ya Elimu, (2004). *Maarifa ya Jamii*.E & D Limited Dar es Salaam.
- Tahenan, M. (2003). Maisha na Mafanikio. Jitambue Media Co. Ltd, Dar es Salaam.
- TUKI, (1985). *Fasihi Simulizi ya Mtanzania, Vitendawili*. Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Dar es Salaam.